# BWANA TUFUMBUE MACHO ILI TUWEZE KUTAMBUA THAMANI YA YESU NA THAMANI YA WOKOVU WETU

## MAANDIKO: LUK. 24: 13-49.

1. **UTANGULIZI**

   Tangu zamani, ujanja/werevu wa shetani kwa wanadamu ni kushughulika na ufahamu wa mwanadamu kwanza kama alivyoshughulika na ufahamu wa mwanamke Hawa; na alipofanikiwa tu kumpofusha fahamu zake; Hawa akatenda tofauti na maagizo ya Mungu na kumkengeusha mumewe jambo lililowafanya wafukuzwe katika Bustani nzuri ya Edeni. ***Mwaz. 3: 1- 7; 24***

- Hadi leo ibilisi vita yake kubwa na wateule waliookoka ni kuhakikisha anawapofusha fahamu zao (akili) ili wasitambue thamani ya wokovu wao; wasahau wema wa Mungu katika maisha yao, na wasahau kabisa ahadi za Mungu ambazo amewaahidi kupitia Neno lake Takatifu!!!
- **Katika kisa hiki cha Cleopa na Mke wake; Yesu anatambua kabisa kwamba shetani tayari amepofusha fahamu zao - *Luka 24: 25.***
- **Baada ya Yesu kutuokoa na kisha tukajawa na Roho Mtakatifu; Yesu anatamani tupate ufahamu wa kutosha wa kulijua kusudi la Mungu la kutuumba kwa mfano wake na kwa sura yake na kututofautisha na wanyama wengine ili tuweze kutawala pamoja naye vitu vyote alivyoviumba pamoja na kumcha yeye peke yake.**
- Shida kubwa ambayo Yesu anawaambia Cleopa na Mkewe hapa; na ambayo ndiyo shida kubwa sana ya Kanisa lake la leo duniani ni ufahamu mdogo tulionao kuhusu kazi kubwa aliyoifanya Yesu pale msalabani; lakini shida ya pili ambayo ni kubwa mno ambayo Yesu aliwakemea Cleopa na mkewe katika safari yao ya kurudi kwao Kijiji cha Emaus ni mioyo mizito ya kuamini yote yaliyonenwa na Manabii!! **Tusome tena. *Luka 24: 25.***
- **Hii ndiyo kanuni ya ibilisi,** anashughulika kwanza na akili za mtu (ufahamu wake) na akifaulu hapa; tayari amemaliza kazi, (moyo mzito maana yake ni ule utashi wa mtu; (uwezo wake wa kufanya maamuzi) ya kumtii Mungu unabadilika;

anajaa hofu na wasiwasi pamoja na kukata tamaa kama Cleopa na Mkewe walivyokuwa wamekata tamaa kabisa na kuamua kurudi Kijijini kwao – ***Luka 24: 14 – 24;*** (**Haya ni maneno ya watu waliokata tamaa na kupoteza imani kabisa kwa Yesu.)**

*Note*: **Shetani kama bingwa wa kupofusha fikira za Wateule wa Mungu, anaweza kukuacha na maandiko uliyoyakariri akilini mwako tu. Mfano:- *Yoh. 19: 28 – 30, 1Petro- 2: 24, Mark. 9: 23, Yer. 32: 27* n.k. lakini kuyaamini kama yalivyo na kuchukua hatua za kuyaishi likawa jambo gumu; ingawa kila yakihubiriwa au kushuhudiwa, moyo unawaka!!! Luka 24: 31 – 32.**

- Katika eneo hili la **kujitambua** sisi ni akina nani na Yesu ni nani na ukuu wake ukoje kwetu shetani anapambana na sisi sana tusilitambue na ndiyo sababu hata sisi wenyewe ambao tunakiri kwamba tumeokoka; hatujitambui, na wala hatutambui kwa kina ushindi wa Bwana wetu Yesu Kristo dhidi ya shetani baada ya kufufuka, ndiyo maana bado tunatembea tukiwa tumejaa hofu na wasiwasi tele!! Shetani amepofusha tu fikira zetu!! ***2Kor. 4:4.*** Ndugu Cleopa na mke wake wanatembea na Yesu masaa mawili na wanazungumza naye lakini hawamtambui!! **They saw him; walk with him, spoke with him but they did not recognize him!!** Hiki ndicho shetani anachofanya hata leo; tunatembea naye mioyoni mwetu, tunamwimbia, tunamtolea sadaka na zaka zetu, lakini kwa asilimia kubwa hatufahamu utendaji wake kwetu. **Mark. 4: 35- 41.** Bila Yesu Kristo (Roho Mtakatifu) kutufunulia/kutufungua ufahamu wetu; kamwe hatutaelewa maana halisi ya maandiko haya. **Luk. 24: 44 – 45.**

**Ampl. Bible- Luke 24: 45 – *Then He thoroughly opened up their minds to understand the scriptures.***

- **Kutofunguliwa ufahamu wetu ili tupate kuelewana na maandiko limekuwa tatizo kubwa ambalo adui shetani amelitumia sana kupoteza wengi. Mt. 22: 23 – 29.**

2. Macho ya mtu yanapofumbwa na adui asitambue ukuu wa Yesu linakuwa ni jambo la hatari sana!! ***Luk.24:15-16*** (ndugu Cleopa na mke wake) wanakunja nyuso zao pale Yesu anapozungumza nao jinsi maandiko yanavyosema kwa habari zake; **Lakini macho yao yalipofumbuliwa na Yesu kutoweka mbele yao, ndipo walipoona jinsi mioyo yao ilivyokuwa ikiwaka wakati Yesu alipokuwa ananena nao na kisha wakarejea Yerusalemu. Ashukuriwe Bwana aliyewapa neema ndugu hawa Cleopa na Mkewe kurejea Yerusalemu, baada ya mioyo yao kuwasuta; kwani wapo wengi leo hata mioyo yao inapowasuta; wanaona aibu kurejea (wanaogopa kutubu kwa kuwahofu wanadamu kwamba watawaonaje**!! Mtu yeyote akifunguliwa ufahamu wake sawasawa na Bwana Yesu, hataogopa wanadamu tena maadamu hawana Mbingu, lazima atachukua hatua za kumfuata Yesu na kufanya mapenzi yake hata kama ni kwa gharama ya kupoteza maisha haya ya mwili huu (kufa) –***Mdo. 21: 9 – 14.***

***Note:*** **Mtu yeyote aliyeokoka, anapotenda jambo lolote lililo kinyume na Neno la Mungu; hatua ya kwanza ni moyo wake kumsuta kama ambavyo Adamu na Hawa mioyo yao ilivyowasuta baada ya kula tunda la mti ambao Mungu alikuwa amewazuia wasile, ndivyo alivyo mteule yeyote hadi leo, akitoka tu nje ya ndoa yake, moyo wake unamsuta; akiiba zaka, akisema uongo, akipokea rushwa, akifanya uasherati, akitoa mimba, akifira, akipiga kunyeto n.k** moyo wake unawaka moto (unamsuta); na hata Neno linapokuwa linahubiriwa!!! **Dawa ndugu zangu ni kuwa kama Cleopa na Mkewe walivyofanya na kurejea Yerusalemu na**

**wakapona. Pata ufahamu huu sasa, usishupaze shingo kwa hofu ya kulinda heshima yako!!!**
**Note: shetani leo hatatumia nyoka ili kunena maneno yatakayo kufumba macho (ufahamu) wako ili umkosee Mungu, atatumia watu, tena walio karibu sana na wewe; kama huna macho ya kiroho (ufahamu wa kujitambua) kwa vyovyote vile utajuta baadaye. Cleopa na mkewe kama macho yao yasingefumbuliwa ndiyo tayari walikuwa wanarudia dini zao na kuiacha neema ya wokovu.**

***Mfano: Neh.6:10-13.*** Kama Nehemia asingekuwa anajitambua, (kama ufahamu wake usingefungulia) maneno haya mazuri ya Shemaya rafiki yake aliyekuwa ameajiriwa na Sanibalati na Tobia yangaliua kabisa juhudi zake zote za kujenga ukuta wa Yerusalimu.

(**au) *2Samwl. 17:5-14.*** Kama Absalomu angetambua kwamba lengo la ushauri wa Hushai Mwarki kwake ni kumwokoa Mfalme Daudi, asingepuuza ushauri wa Jemedari Ahithofeli; aliokuwa ametangulia kuutoa kwake.***2Samwl.16:20-23, 17:1-4***

**(au) Nabii kijana**. ***1Wafal. 13:11-22***. Kama angetambua (kama angefahamu) kuwa lengo la nabii mzee kumpa ushauri ule ni kumwangamiza, asingeenda kula nyumbani kwake, bali angesimama na maelekezo ya Mungu alivyokuwa amempa. Lakini akapofushwa na neno "mimi nami ni nabii kama wewe, na Malaika akaniambia kwa neno la Bwana mrudishe ale chakula na anywe maji!! ***Mst. 18***

**(au) Yusufu**. ***Mwaz.39:6-12.*** Alipotambua (alifahamu) kwamba ushauri wa mke wa Potifa lengo lake ni kumfanya amkose Mungu; Yusufu akakimbia na kujiokoa nafsi yake jambo lililomfanya adumishe urafiki na uhusiano wake na Mungu. Ufahamu wa jinsi hii alikuwa nao pia Daniel na wenzake-***Dan.1:5-8, Mordekai- Est 3:1-6 n.k***

**(au)** **Amnoni** . ***2Samwl. 13:1-17, 26-30*** ushauri wa rafiki yake Abinadabu ndiyo uliopelekea kifo chake; kama angekuwa na macho (ufahamu) wa kutambua madhara ya ushauri huo angejiokoa. Wakati mwingine ushauri unakufanya/unauchochea moyo uwake kabisa katika kwenda kutenda maovu !! ***2 Samwl. 16:20-23!***!! ***Hapa nakumbuka mtu mmoja aliyempa mwanangu Mosses Tshs. 500/- tu na kumchochea akapigane!!***

***Note: Ushauri huu wa Ahithofeli kwa Abusalomu ni sawa na ushauri wa waganga wa kienyeji wengi leo; ulipofusha kabisa ufahamu wa Absalom!! Ni sawa na ushauri wa manabii wengi wa uongo leo; watu wanatembea kabisa na chumvi, mafuta,maji, utadhani wamepagawa, hawaambiliki, wamepofushwa kabisa akili zao, wanavuliwa nguo lakini hawashtuki kamwe***!!!

**(au)** **Akani** *Yosh.7:1* au **Yuda-** *Math. 26:14-16, 27:3-5* au **Anania** na **Safia** *Mdo.5:1-11*, au **Kora na wezake.** ***Hes.16:1-35*** n.k unakuwa katika Kanisa na wengine lakini adui anakupandia roho ya ubinafsi na majivuno na kudharau wengine, au anakupandia roho ya wizi wa kumwibia Mungu akupaye uzima na ulinzi wake bure; unapotelea ndani ya kanisa kwa sababu ya kupofushwa fikira zako na ibilisi!!!

3. Bwana akitufungua macho (ufahamu) na kutambua kwa kina thamani ya Yesu Kristo; thamani ya Neno lake pamoja na thamani ya wokovu huu tulioupata kwa gharama kubwa iliyolipwa na Bwana Yesu. ***Ebr. 2:3.***

**<u>Tutautunza kwa gharama yoyote na kisha ndipo tutakuwa: Luka 24: 44- 45.</u>**

a. Tutakuwa tunaona mambo yanayoendelea katika Ulimwengu huu kama Mungu mwenyewe anavyoyaona na hivyo kutodanganywa au kutetemeshwa hovyo hovyo na adui. ***2Wafalm. 6:15-17 2Nyak.20:14-22, Kut.14:10-14, Isay 41:8-12***

b. Tutaishi maisha ya ushindi daima na kamwe adui hatatutetemesha ***Yosh.5:13-15, 6:1-22, 2Nyak.32:6-8, na saa ya changamoto hatutapiga yowe- Mark. 4: 35 – 41; bali tutaimba zaburi- Mdo. 16: 23 – 26, Yak. 5:13.***

c. Hatutajivuna wala kujikweza bali wakati wote tutanyenyekea chini ya mkono wa Mungu wetu ***Mdo. 3:11-13, 14:8-18.***

d. Tutazijua siri za Mungu wetu na kamwe hatutatembea gizani. ***Zab. 25:14, 2Wafal.6:8-13*** na wala shetani hatatudanganya kwa urahisi na pia **tutakuwa na jukumu la kuwaimarisha wengine katika imani.** ***Mdo 21:9-14***. Ebu kila mmoja wetu leo atamani Bwana Yesu amfungue macho yake (ufahamu wake) ili apate kufahamu kwa kina kazi kubwa aliyoifanya pale msalabani pamoja na kupokea faida nyingi zinazotokana na kifo cha Yesu Kristo pale msalabani. **Amina**

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***Dec 2021***